Global Schools Program

MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU




# Muhtasari wa Kozi

## Darasa la 7

---

**Chanzo:** Reimers, F. (2017). *Empowering students to improve the world in sixty lessons*. Toleo la kwanza. Createspace Independent Publishing Platform.

**Haki ya kunakili:** © 2017 Fernando M. Reimers. Kazi hii imeidhinishwa chini ya leseni ya kimataifa ya Creative Commons Attribution 4.0. ili kutazama nakala ya leseni hii, tembelea https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/ Haki zote zimehifadhiwa.

**Ilani:** Maudhui yote ya humu yaliandaliwa na kuchapishwa na Global Schools Program.

---

SUSTAINABLE DEVELOPMENT GOALS
17 GOALS TO TRANSFORM OUR WORLD

Global Schools Program

| Muhtasari | |
|---|---|
| **Lengo kuu la Kujifunza**<br>Kwa kuwa wamejifunza nafasi zao katika jamii na ulimwengu kwa ujumla, sasa wanafunzi wataanza kujiona kama waleta mabadiliko. Kwa kujifunza kutoka kwa wanarika wenzao na wanajamii wengine, wanafunzi wataanza kutengeneza mipango ya jinsi gani wataufanya ulimwengu uliowazunguka kuwa mahali bora. | |
| **Nguzo za Somo** | |
| **Somo 1** | Matatizo gani yanayohusiana na Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME) yaliyopo katika nchi yangu? |
| **Somo 2** | Namna gani watu wengine walitatua matatizo haya? |
| **Somo 3** | Namna gani ninaweza kujifunza kutoka kwa waleta mabadiliko wengine? |
| **Somo 4** | Nimejifunza nini kutoka kwa waleta mabadiliko wengine? |
| **Somo 5** | Nini tunachoweza kufanya kwa sasa? |
| **Malengo ya Kujifunza** | |
| • Wanafunzi watatumia mbinu za ufanyaji utafiti kama vile kufanya mahojiano, kuchambua taarifa, na uwasilishaji wa matokeo.<br>• Wanafunzi watafanya kazi katika makundi ili kutatua matatizo kwa ubunifu.<br>• Wanafunzi watafanya mazoezi ya uongozi, huruma na ushawishi. | |

**Darasa la 7 Somo 1**

"Matatizo gani yanayohusiana na Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME) yaliyopo katika nchi yangu?"

**Muda:** Dakika: 60
**Masomo:** Maarifa ya Jamii, Sayansi, Kilimo
**Viwango:** Somo linaweza kutumika katika Malengo ya Maendeleo Endelevu yote 17, kutegemeana na masuala ambayo wanafunzi wanayaona katika mazingira ya jamii zao.
**Limebuniwa na:** Kara Howard

**Muhtasari na Mantiki:** Somo hili linalenga kuingiza Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME) katika mazingira halisi ya wanafunzi. Wanafunzi wataanza kuelewa matatizo wanayoyaona katika jamii zao ambayo ni sehemu ya matatizo ya kimataifa

**Malengo ya Somo:** Wanafunzi watapata umahiri ambao utawawezesha;

- Kuelewa haki za binadamu wote ili kuwa na maisha ya furaha, afya, na kuwa na maisha yenye tija bila kujali jinsi, umri, ulemavu, n.k.
- Kutambua na kukubaliana na hali ya uhuru wa kutegemeana baina ya watu wote, viumbe hai, na sayari.
- Kufahamu juu ya uhaba wa maji, nishati, na chakula.
- Kuunda muundo wa kimaadili juu ya rasilimali zetu na vingine vyote vyenye uhai, juu ya ardhi na kwenye maji, na kuelewa jukumu letu katika kutunza/kuhifadhi sayari yetu kwa ajili ya maendeleo endelevu.
- Kupembua na kufanya utafiti wa kupata suluhisho la matatizo (maji, nishati, na chakula) kutoka katika mitazamo mbalimbali ya kimajukumu ikihusisha, wanunuzi, wafanya biashara, wanasayansi, watunga sera, watafiti, walanguzi, vyombo vya habari, na mashirika ya maendeleo, na wengineo.
- Kuamini kwamba maboresho yanaweza kufanyika kupitia mtazamo wa kimaendeleo.

**Malengo ya Uelewa:** Wanafunzi watakuwa na uwezo wa kuona uhusiano uliopo baina ya matatizo yaliyopo katika jamii zao na masuala makubwa ya kiulimwengu ambayo Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME) yanalenga kuyashughulikia.

**Maswali ya  Muhimu:**

- Yapi ni matatizo sugu tunayoyaona katika jamii yetu?
- Kwa namna gani matatizo haya yanaingia katika mfumo mpana wa kiulimwengu?
- Kwanini unafikiri matatizo haya yapo katika jamii zetu na ulimwenguni?

**Malengo ya kujifunza kwa mwanafunzi (wanafunzi watakuwa na uwezo wa):**

- Kutambua matatizo makubwa katika jamii zao
- Kuhusianisha matatizo haya na yale yaliyoelezwa katika Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME)
- Kujadili kwanini matatizo haya yapo katika jamii zao

**Upimaji:**

- Mwalimu atafanya upimaji usio rasmi ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wanafikiri kwa umakini juu ya matatizo wanayoyabaini, kutoa ushahidi kuwa wameyaona matatizo hayo, na kwanini wanafikiri matatizo hayo yapo katika jamii yao.
- Kama mwalimu anaona kuna umuhimu wa upimaji rasmi, anaweza kufanya upimaji kwa kuwataka wanafunzi kuhusianisha matatizo waliyoyabaini katika jamii zao na Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME).

**Mtiririko wa shughuli:**

- **Utangulizi:** Mwalimu atatambulisha Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME) kwa wanafunzi. Mwalimu ataelezea kuwa ni malengo tuliyoweka ili kutambua ajenda za kuwekea mkazo katika kuboresha dunia yetu ifikapo 2030. Mwalimu atayaandika malengo 17 chini na kuwataka wanafunzi kujadili kama wanadhani malengo haya ni muhimu:

❖ Kutokomeza Umasikini wa aina zote
❖ Viwanda, Uvumbuzi na Miundombinu
❖ Kutokomeza njaa, kuwa na uhakika wa chakula
❖ Kuwepo na usawa wa kijinsia
❖ Kuhakikisha afya njema na ustawi wa watu
❖ Miji na jamii endelevu
❖ Kuhakikisha elimu bora, yenye usawa
❖ Uwajibikaji wa uzalishaji na matumizi
❖ Usawa wa kijinsia
❖ Kuchukua hatua kuhusu tabianchi
❖ Kuhakikisha upatikanaji na usimamizi endelevu wa maji na usafi kwa wote.
❖ Uhai wa viumbe vya majini
❖ Ushirikiano juu ya malengo
❖ Nishati mbadala kwa gharama nafuu
❖ Kulinda uhai wa viumbe wa nchi kavu

- ❖ Ajira zenye staha na ukuaji kiuchumi
- ❖ Amani, haki na taasisi imara

- **Shughuli:**
    - Wakiwa na malengo haya akilini, wanafunzi watakaa katika makundi madogo madogo ili kujadili matatizo wanayoyaona katika jamii zao wenyewe. Ni lazima wanafunzi watengeneze orodha ya matatizo waliyoyabaini pamoja na ushahidi wa kuwepo kwa matatizo hayo.
    - Pia, ni lazima wanafunzi waanze kuunda nadharia juu ya kwanini wanafikiri hayo matatizo yapo katika jamii. Mwalimu lazima azungukie makundi ili kuwasaidia katika uundaji wa nadharia za matatizo na pia kuwasaidia kuyahusianisha na Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME).

- **Hitimisho:** Itawalazimu wanafunzi katika makundi hayo madogo madogo kuwasilisha orodha zao za matatizo mbele ya darasa. Kama muda utaruhusu, wanafunzi watajadili kwa pamoja kama darasa matatizo wanayohisi yana shinikizo zaidi.

**Darasa la 7 Somo 2**

"Fanya tafiti kwa watu kwenye jamii ambayo ni ya waleta mabadiliko"

**Muda:** Dakika: 60
**Masomo:** Maarifa ya Jamii, ELA
**Viwango:** Somo linaweza kutumika katika Malengo ya Maendeleo Endelevu yote 17, kutegemeana na masuala ambayo wanafunzi wanayaona katika muktadha wa jamii
**Limebuniwa na:** Chloé Suberville

**Muhtasari na Mantiki:** Somo hili linakusudia kuwawezesha wanafunzi kuwatambua watu katika jamii yao ambao tayari wamepiga hatua kuelekea mabadiliko waliyoyabaini katika somo lililopita.

**Lengo la Somo:** Wanafunzi watatengeneza orodha ya watu wote wanaowajua au waliowasikia katika jamii zao walioleta mabadiliko katika jamii yao ili wawe mfano wao ili kuwahoji, kama hatua ya msingi wa kuelekea kuwa mawakala wa mabadiliko katika miji yao wenyewe, mikoa na nchi.

**Malengo ya Uelewa:** Wanafunzi watakuwa na uwezo wa kuelewa nini kinamtambulisha mtu ambaye ni mleta mabadiliko na kuunganisha wazo hilo na watu waliopo katika jamii yao.

**Maswali ya muhimu:**

- Nini kinamtambulisha mtu kama wakala wa mabadiliko?
- Je, tunajuaje aina ya mabadiliko wanayoyaleta/kuyafanya?
- Nani ni mawakala wa mabadiliko tunaowajua ulimwenguni kote?
- Vipi kuhusu katika jamii zetu?

**Wanafunzi watakuwa na uwezo wa:**

- Kuelewa nini kinamtambulisha/kumfanya mtu fulani kuwa wakala wa mabadiliko
- Kujua aina za mabadiliko ambayo mtu binafsi anaweza kuwa anafanyia kazi
- Kuangalia watu kwenye maisha yao na kutambua aina ya mabadiliko wanayoyapambania katika udogo au ukubwa wake

**Upimaji:** Je, wanafunzi wamefanikiwa kutambua angalau mtu mmoja katika jamii ambaye watawasiliana naye na kumhoji kwa lengo la kubaini kama ni wakala wa mabadiliko katika jamii yao?

**Mtiririko wa shughuli:**

- Wakumbushe wanafunzi kwamba wakala wa mabadiliko anaweza kuwa na mtazamo wa njia tofauti tofauti. Fikiri juu ya somo lililopita na njia ambazo tuliainisha matatizo katika jamii yetu. Waelekeze wanafunzi kuwafikiria mawakala wa mabadiliko katika ulimwengu lakini pia katika jamii zetu ili kusudi tuweze kuwasiliana nao na kuwatumia kama mfano wa kuigwa.

- Wanafunzi watageukiana na kuzungumza kuhusu wakati ambapo waliwaona watu waliokuwa mawakala wa mabadiliko na walivutiwa sana katika hali fulani. Mwalimu azunguke wakati wanafunzi wanazungumza na kuandika baadhi ya maudhui yaliyojadiliwa. Lilete darasa kwa pamoja na chagua baadhi ya wawakilishi waweze kuwasilisha kile walichojadili. Zungumzia maudhui tofauti tofauti ambayo unayajua na uyafungamanishe katika maudhui mapya yaliyojadiliwa na wanafunzi.

- Wape wanafunzi muundo wa michoro wa visanduku (graphic organizer) na uwaambie wavijaze kwa kutumia mtu wanayefahamiana naye (sio mtu maarufu, bali mtu wa kwenye maisha yao).

- Wanafunzi waende na mchoro wa visanduku nyumbani na kuzungumza kwa pamoja na watu wao ambao ni mfano wa kuigwa, au mtu yeyote wanayedhani anaweza kuwa wakala wa mabadiliko katika jamii yao ili waanze kuzungumza nao kuhusu hili.

- Darasani, wanafunzi wanaweza kufanya kazi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kujadili majibu yao. Wanafunzi wengine ni lazima watoe mwitiko (feedback): waseme kipi ni kizuri katika michoro ya visanduku na wafanye nini ili kuiboresha.

- Baada ya kukamilisha michoro ya visanduku, wanafunzi wataandika aya za maelezo kwa kutumia taarifa walizokusanya na michoro yao ya visanduku. Halafu, wanaweza kurudi tena katika makundi yao ya wanafunzi watatu watatu na wenzao wawape mapendekezo.

- Sambaza rasimu za mwisho za aya zao ili wanafunzi wote wasome kazi za wenzao kila mmoja. Kisha warudishe katika mkao wa darasa ili kujadili maswali yafuatayo:
    - Maudhui gani yamejirudia katika uandishi wa wanafunzi wenzao?
    - Kuna mfanano gani kati ya wakala wa mabadiliko wenzao walio wazungumzia na watu wa kihistoria wanaowafahamu?

- Zipi ni tofauti?
- Nini ulichojifunza kutoka kwenye zoezi hili ambacho kinahamasisha watu wafanye kazi kuleta mabadiliko na wanaendeleaje kufanya hivyo?

**Nyenzo kwa walimu:**

- Muundo wa mtu ambaye ana kuhamasisha: https://www.learningforjustice.org/sites/default/files/general/L3%20Role%20Model%20Graphic%20Organizer%206-8.pdf
- Mawakala wa mabadiliko katika maisha yetu: https://www.learningforjustice.org/classroom-resources/lessons/change-agents-in-our-own-lives

**Darasa la 7 Somo 3**

"Mahojiano na kuuliza maswali"

**Muda:** Dakika: 60
**Masomo:** Maarifa ya Jamii, Elimu ya Uraia
**Viwango:** Amani, Haki, na Taasisi Imara (MME 16). Malengo mengine yanaweza kujumuishwa kulingana na maslahi maalum ya wanafunzi na jamii wanayoishi.
**Limebuniwa na:** Nicolás Buchbinder

**Muhtasari na Mantiki:** Wanafunzi watajifunza kuhusu namna ya kuendesha mahojiano kwa lengo la kuendesha mahojiano yao wenyewe na waleta mabadiliko katika jamii zao.

**Lengo la Somo:** Wanafunzi wataelekezwa namna ya kuendesha mahojiano ili kupata taarifa muhimu za kuibadilisha jamii.

**Malengo ya Uelewa:**

- Wanafunzi watajifunza kumhoji mleta mabadiliko katika jamii zao kama sehemu ya mchakato wa kuelewa jinsi watu wanavyofanya mabadiliko katika jamii.
- Wanafunzi katika somo hili watazingatia juu ya maswali gani ya kuuliza na namna ya kufanya mahojiano.

**Maswali Muhimu:**

- Maswali gani muhimu ya kumuuliza mleta mabadiliko kwenye jamii yangu?
- Nawezaje kuyapa kipaumbele maswali ya muhimu?

**Malengo ya kujifunza kwa Mwanafunzi (wanafunzi watakuwa na uwezo wa):**

- Kujihusisha katika kufikiri maswali ya kuwauliza waleta mabadiliko katika jamii yao
- Kufanya mazoezi na kupata mwitiko juu ya kufanya mahojiano
- Kuunda itifaki ya mahojiano

**Upimaji:** Mwalimu atachochea ushiriki kama njia isiyo rasmi ya kumfanyia tathmini kila mwanafunzi; mwalimu atakusanya itifaki zilizoundwa na wanafunzi.

**Mtiririko wa shughuli:**

- **Kufungua (Dakika: 5):**
    - Mwalimu atawauliza wanafunzi kukumbuka mazoezi waliyoyafanya katika kipindi kilichopita na kuwataja wanajamii tofauti tofauti ambao waliwabainisha kama waleta mabadiliko.

- **Kuwasiliana na mhojiwa (anayehojiwa) (Dakika: 10):**
    - Mwalimu ataelekeza kundi zima la wanafunzi jinsi gani wanaweza kuwasiliana na mleta mabadiliko. Watapitia mbinu mbalimbali za kufanya hivyo: barua pepe, simu, au mawasiliano ya ana kwa ana , n.k.
    - Darasa litakubaliana kuhusu njia bora zaidi ya kuwasiliana na mhojiwa kwa ajili ya mradi.

- **Maswali (Dakika: 15):**
    - Mwalimu atawagawanya wanafunzi katika makundi tofauti. Kila mmoja wao atafikiria maswali 10 wanayotaka kuwauliza waleta mabadiliko katika jamii zao.
    - Baada ya hapo, darasa litajadili kwa ufupi maswali muhimu anuai na mwalimu atayapangilia maelezo hayo katika vipengele mbalimbali muhimu:
        - Historia binafsi ya mhojiwa
        - Eneo la kutilia maanani
        - Juhudi za uhamishaji
        - Vikwazo vya mabadiliko ya kijamii
        - Matokeo ya shughuli
        - n.k.

- **Mazoezi ya Mahojiano (Dakika: 20):**
    - Mwalimu ataigiza kama mhojiwa na kuchagua wanafunzi kadhaa kwa ajili ya mahojiano. Watapitia baadhi ya maswali waliyokubaliana katika zoezi lililopita.
    - Baada ya dakika 5, darasa litachangia kwa ufupi kuhusu uzoefu wa mahojiano hayo, na kuzungumzia mgawanyo wa nafasi katika mahojiano na zana za maandalizi (maandishi, sauti zilizorekodiwa, usikilizaji wa makini, maswali ya ufuatiliaji).
    - Baada ya hilo, mwalimu atachagua wanafunzi wengine wawili na kuigiza tena, wakati huu ataigiza kama mhojiwa “katili” (ambaye hazungumzi sana, anayezungumzia kitu tofauti na alichoulizwa, n.k.)

- Baada ya dakika 5, mwalimu atawatahadharisha wanafunzi juu ya uwezekano wa kuwa na mhojiwa wa aina hii.

- **Uundaji wa Itifaki (Dakika: 10):**
    - Wanafunzi watatumia dakika 10 za mwisho za kipindi kuunda itifaki ya mahojiano, ambapo wataeleza wao ni nani, kwanini wanataka kufanya mahojiano, wataomba kibali cha kurekodi, na kuchagua maswali 6-8 ya kuuliza.

**Nyenzo kwa walimu:**

- https://thoughtfullearning.com/inquireHSbook/pg346
- https://studentreportinglabs.org/lesson-plans/lesson-2-2-interviewing-the-art-of-asking-questions/
- https://www.myworldofwork.co.uk/sites/default/files/mock-interviews-activity.pdf

**Darasa la 7 Somo 4**

"Nini kinamtambulisha mleta mabadiliko? Kujifunza kutoka kwa viongozi wa mabadiliko"

**Muda:** Dakika: 60
**Masomo:** Maarifa ya Jamii, Uraia, Kusoma, Sanaa ya Lugha
**Viwango:** Somo linaweza kutumika katika Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME) yote 17 kutegemea na masuala ambayo wanafunzi wanayaona katika muktadha wa jamii yao.
**Imeandaliwa na:** Tatiana Shevchenko

**Muhtasari na Mantiki:** Somo hili linalenga kuwasaidia wanafunzi kuelewa zaidi sifa za waleta mabadiliko kwa kupitia walichokipata kutokana na mahojiano yaliyofanyika na waleta mabadiliko.

**Malengo ya uelewa:**

- Wanafunzi watatumia mawazo ya uchanganuzi wa hali ya juu ili kuelewa sifa za mawakala wa mabadiliko na kulinganisha na sifa zao wenyewe, hivyo kuelewa kwamba wao pia wanaweza kuwa mawakala wa mabadiliko.
- Wanafunzi watatumia michoro maandishi kama zana maono, kuweza kupanga na kuchambua taarifa kutoka kwenye mahojiano.
- Wanafunzi wataunda kielelezo cha veni cha darasa ili kulinganisha na kuweka ulinganifu baina ya wahojiwa wao kwa wao kwa ajili ya kuelewa zaidi na kuwasilisha walichojifunza baada ya kufanya mahojiano.

**Malengo ya Somo:**

- Baada ya kufanya mahojiano wanafunzi watawasilisha kile walichokipata kwa darasa.
- Wanafunzi watajifunza aina mbalimbali za waleta mabadiliko, haiba zao na wasifu wao.
- Wanafunzi watachambua vitu gani wafanye ili wawe waleta mabadiliko na watachunguza kwa undani athari zinazoletwa na mtu mmoja anaweza kuwa nayo kwa maisha ya watu wengine. Vilevile, wanafunzi wataelewa kuwa wao pia wanaweza kuwa waleta mabadiliko.

**Maswali muhimu:**

- Watu gani wanaoleta mabadiliko?
- Mienendo na tabia za waleta mabadiliko ni ipi?
- Ni kwa jinsi gani wanaoleta mabadiliko wanafanana au kutofautiana?
- Nini kinawahamasisha watu kuchukua hatua?
- Zipi ni aina za hatua anazoweza kuchukua/kufanya mleta mabadiliko?
- Jinsi gani upeo wa hatua za waleta mabadiliko unatofautiana?

- Ni changamoto gani watu hawa wanakutana nazo?
- Namna gani matendo ya mtu yanaweza kuleta athari katika jamii yake/ulimwengu?
- Tunaweza kujifunza nini na kwa jinsi gani kutoka kwenye maisha ya wengine?
- Jinsi gani sisi wenyewe tunaweza kuwa waleta mabadiliko?

**Malengo ya kujifunza kwa mwanafunzi (wanafunzi watakuwa na uwezo wa):**
- Kujenga uelewa wa kile kinachomtambulisha mleta mabadiliko na jinsi gani sifa za mleta mabadiliko zinaweza kufanana au kutofautiana na za kwao.
- Kuelewa kwamba wao pia wanaweza kuwa waleta mabadiliko.
- Kuongea kwa ufanisi na kifupi kuelezea walichokipata kutoka kwenye mahojiano.
- Kutumia mbinu ya michoro maandishi kupangilia na kuchambua walichojifunza na kuchanganya na vingine.
- Kuwasikiliza wanarika wenzao na kulinganisha na kutofautisha majibu waliyopata.
- Kufanya kazi katika vikosi vidogo na vikubwa ili kufanikisha majukumu ya pamoja.
- Kutengeneza kwa ubunifu michoro na kusambaza taarifa nyingi zilizofupishwa kwa urahisi.

**Upimaji:** wanafunzi watapimwa kulingana na:
- Ushiriki wao katika hadithi simulizi
- Kupangilia/kuandaa  taarifa za kwenye mchoro wa maandishi kwenye bango
- Uwasilishaji
- Ushiriki katika zoezi la mchoro wa veni.

*Ushiriki hai utawahitaji wanafunzi kuwasilisha mawazo yao, kusikiliza mawazo ya wengine na kuchangia katika mjadala wa darasa.*

**Mtiririko wa shughuli:**

- **Utangulizi (Dakika: 5):**
    - Mwalimu atawagawa wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu . Wanafunzi wamefanya mahojiano na waleta mabadiliko na wako tayari kuwasilisha walichokipata.
    - Wanafunzi watapewa maelekezo ya kuwasilisha mahojiano yao kwa kila mmoja ndani ya vikundi vidogo. Wanapowasilisha wataelekezwa kuwalinganisha na kuwatofautisha waleta mabadiliko wao.
    - Wanafunzi wafanye kazi kama kundi na kuweka vielelezo vya matokeo ya tafiti kwenye bango wakitumia michoro ya maandishi na kisha wataambiwa kwamba,

baada ya vikundi vidogo kumaliza uwasilishaji kwa wenzao darasa litafanya kazi kwa pamoja kuandaa mchoro wa veni wa mleta mabadiliko, ambapo darasa litachambua jinsi gani tabia za mleta mabadiliko na za wanafunzi wa darasa la saba zinafanana.

- **Kuhusisha na Michoro Maandandishi (Dakika: 20):** Katika vikundi vya wanafunzi watatu (3). Wanafunzi wafanye kazi ya kumuwasilisha mhojiwa wao. Wanafunzi watapewa kazi ya kuunda bango la michoro maandishi (sketchnotes) yenye taswira ya tabia za waleta mabadiliko. Pale ambapo makundi yatamaliza mabango yao watayaweka juu sehemu mbalimbali darasani.

- **Uwasilishaji wa bango (Dakika: 10):** Kila kikundi (watu wa 3 kila kikundi kulingana na darasa la watu 30) watachukua dakika 1 kuwasilisha bango lao, kudokeza vitu vya msingi kutoka kwenye mjadala wao wa kikundi.

- **Kielelezo cha veni cha darasa (Dakika: 20):** Wanafunzi wafanye kazi pamoja kutengeneza kielelezo kikubwa cha veni ambacho kinaonesha (kwa kufananisha na kutofautisha) sifa za mawakala wa mabadiliko waliohojiwa na wanafunzi darasani.

    - **Mfano wa watu ambao wanaweza kuwekwa kwenye kielelezo cha veni:**
        - Ni wa kwanza kuchukua hatua
        - Wakati mwingine wanakumbana na hali ngumu
        - Waliopitia vipingamizi mwanzoni
        - Wanaoendeleza mawazo yao binafsi
        - Watu wanaowakusanya wengine kwenye mambo ya kiimani
        - Wenye imani kali

    - **Mfano wa watu ambao wanaweza kujumuishwa kwenye sehemu ya mwingiliano katika kielelezo:**
        - Wenye nguvu
        - Wenye matumaini
        - Wenye tamaa ya makuu
        - Ni sehemu ya jamii
        - Wenye ndoto
        - Wenye uwezo wa kujifunza vitu vipya na kupangilia mawazo

- **Mfano wa watu ambao wanaweza kujumuishwa kwenye upande wa kielelezo wa darasa la saba:**
  - Wanawategemea walezi wao
  - Mara zote hawana nyenzo sahihi (pesa, muda)
  - Hawawezi kuwashawishi kirahisi watu wazima ambao mara kwa mara hufanya maamuzi

- **Hitimisho (Dakika: 5):** Mwalimu ataonesha kwamba waleta mabadiliko na dhamira zao zinaweza kuonekana kama tofauti sana, lakini wana sifa nyingi zinazofanana wao kwa wao na vilevile na wanafunzi humo darasani. Mwalimu pia ataonesha sifa za wanadarasa ambazo zinatofautiana na za waleta mabadiliko na kwamba inawezekana kujifunza na kuendelezwa. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutafakari hili kabla ya kipindi kijacho.

**Nyenzo kwa wanafunzi:**

- wanafunzi watahitaji kalamu na makaratasi ya mabango; zana zaidi zinaweza kutolewa (gundi, mikasi, majarida kwa ajili ya kukata picha, mapambo ya mng'ao, riboni, n.k.)
- Kama wanafunzi walitumia vifaa vya kurekodia video (kamera, simu, kompyuta) ili kukusanya na kusambaza mahojiano, vifaa hivyo inabidi viwemo darasani.

**Nyenzo kwa walimu:**

- http://unmasadalha.blogspot.com/2016/01/venn-diagram.html
- https://ditchthattextbook.com/sketch/
- https://livinginthelayerscom.wordpress.com/2018/02/04/visual-notetaking-and-analysis-of-poetry-with-sketchnoting/

**Darasa la 7 Somo 5**

"Kutazamia mabadiliko ya wakati ujao"

**Muda:** Dakika: 60
**Masomo:** Maarifa ya Jamii, Sayansi
**Viwango:** Uboreshaji Usawa (MME 10); Amani, Haki na Taasisi Imara (MME 16); Ushirikiano wa Malengo (MME 17)
**Limebuniwa na:** Katherine Kinnaird

**Muhtasari na Mantiki:**

- Kutokana na mahojiano waliyoyamaliza na uwasilishaji, wanafunzi wataweza kuchunguza njia ambazo zitawawezesha kuwa waleta mabadiliko katika jamii zao na ulimwengu kwa ujumla.
- Katika hatua hii muhimu katika elimu yao, watajifunza namna ya kutumia maarifa ambayo wameyapata katika masomo na maisha yao ya baadaye.

**Malengo ya Somo:**

- Wanafunzi watajifunza jinsi ya kutambua suala muhimu la kijamii na namna ya kufanya kazi na wanafunzi wengine ili kutengeneza mpango wa utaratibu kwa ajili ya kutatua suala hilo katika siku zijazo.
    - Katika Maarifa ya Jamii, watapata uelewa wa masuala ya haki za kijamii.
    - Katika Sayansi, watatumia njia za kisayansi kutambua tatizo, kufanyia utafiti, kudhania utatuzi, kujaribu utatuzi wao, kuchambua matokeo, kuelezea utatuzi na kueleza kwa wengine mpango kazi wa kijamii mbele ya darasa.

**Malengo ya uelewa:**

- Wanafunzi wataelewa umuhimu wa kufanya kazi kwa umoja ili kuleta mabadiliko.
- Wanafunzi watapata ujuzi wa ushirikiano, utafiti, uchambuzi na mawasiliano.
- Wanafunzi watapata changamoto na pongezi zinazotokana na kazi ya ukarabati wa jamii.

**Maswali muhimu:**

- Masuala gani jamii yangu inakabiliana nayo?
- Masuala gani ulimwengu unakabiliana nayo?
- Je, masuala haya yako sawa na yale ya kwenye jamii yangu?
- Namna gani masuala haya yote ya kijamii yanaingiliana?
- Ni yupi kati ya wanafunzi wenzangu aliyefanyia utafiti kila suala?
- Ninaweza kufanya kazi na nani ili kuleta mabadiliko?

**Malengo ya Mwanafunzi  Kujifunza (wanafunzi watakuwa na uwezo wa):**

- Kufanya kazi na kuwasiliana kwa ufanisi na wanafunzi wenzao.
- Kuelezea mawazo yao kuhusu masuala muhimu ya kijamii
- Kufikiri kwa kina kuhusu namna ya kutatua masuala ya kijamii
- Kuandaa mpango kazi wa kijamii kwa ubunifu na kisayansi

**Upimaji:** Mbinu za kujifunza (ATL) za mfumo wa mtaala wa International Baccalaureate (IB) kwa programu ya madarasa ya kati (MYP):

- **Kuanza/Novice (N)** — Wanafunzi wanaanza kuelewa utafiti na mchakato wa ushirikiano lakini hawachukui majukumu katika uundaji wa mpango kazi wa kijamii.

- **Kuendeleza/Learner (L)** — Wanafunzi wanafanya kazi na wengine na kushiriki katika uundaji wa mpango kazi wa kijamii kupitia msaada wa mara kwa mara kutoka kwa mwalimu.

- **Utumiaji/Practitioner (P)** — wanafunzi wanafanya kazi vizuri katika makundi yao na kuwasilisha kwa kujiamini mpango kazi wao mbele ya wanafunzi wengine darasani.

- **Mtaalam/Expert (E)** — wanafunzi ni viongozi katika makundi yao na wanawasaidia wanafunzi wanaohangaika. Kwa ujasiri wanauelezea mbele ya darasa mpango kazi wa kijamii na umuhimu wake hapo baadaye.

**Mtiririko wa shughuli:**

- **Shughuli ya Ufunguzi:**
    - Wanafunzi wanafikiria masuala yote ya kijamii ambayo wameyatafiti katika mahojiano yao. Wanatengeneza orodha moja kuhusu masuala yanayoikumba jamii yao na mengine yanayoukumba ulimwengu.
    - Wanafunzi wanatambua ni wapi ambapo masuala yanayoikumba jamii na yanayoukumba ulimwengu yanaingiliana. Kutokana na uchambuzi wa masuala ya msingi, wanafunzi watajigawa katika makundi ili kujadili/kutatua tatizo mojawapo.
    - Zingatia: ni muhimu kwamba wanafunzi wajigawe wenyewe katika makundi kuliko mwalimu awagawe, kwa sababu wanahitaji kujifunza kutengeneza uhusiano kati ya mada zao za mahojiano ya utafiti na mada za wanafunzi wenzao. Mara ambapo wanafunzi watajigawa mwalimu atathibitisha makundi na kufanya mabadiliko yoyote pale inapobidi.

- **Shughuli kuu:** Kama kikundi wanafunzi watatumia njia za kisayansi kutambua tatizo ambalo wataligusia, watatoa mawazo yao kuhusu tatizo kutokana na mahojiano ya utafiti wao, kuweka nadharia ya utatuzi wa tatizo, kufikiria matatizo na mafanikio yanayoweza kujitokeza kutokana na utatuzi, kuchuja utatuzi na kuandaa mpango kazi.

- **Shughuli ya kufungia:** Wanafunzi waeleze mbele ya darasa mchakato walioufikiria na mpango kazi wao wa mwisho.

**Nyenzo kwa wanafunzi:**
- Hatua za njia za kisayansi: https://www.sciencebuddies.org/science-fair-projects/science-fair/steps-of-the-scientific-method

**Nyenzo kwa walimu:**
- Masuala ya kiulimwengu: https://www.globalissues.org/